

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

MACHI 2017

AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

YALIYOMO:

1. LENGU LA MADA

2.UTANGULIZI

3.MAANA YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

4.FAIDA ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

5. NJIA BORA ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

1. Lengo la Mada

-Kuhakikisha mazingira ya miundombinu ya miradi ya maji yanakuwa safi

-Kuepusha Magonjwa yanayoambukizwa kutokana na uchafu au maji yasiyo salama.

2. Utangulizi

Pamoja na kuwezesha upatikanaji wa huduma ya maji safi, Mradi wa Maji unaleta faida za kiafya kama vile kupunguza magonjwa ya tumbo na kuharisha. Faida hizo zinaweza kupatikana endapo miradi hiyo mipya

itaambatana na matumizi sahihi na salama ya maji hayo pamoja na utunzaji wa mazingira ya miundombinu, mfano kuzingatia usafi katika vituo vya kuchotea maji.

3. Maana ya Afya na Usafi wa Mazingira

Usafi wa Mazingira ni mchakato wa shughuli zenye kulenga kuwa na mazingira yatakayoweza afya bora. Kwa mtazamo wa miradi ya maji, usafi wa mazingira unajumuisha uwekaji na kuwa na matumizi sahihi ya miundombinu ili kuzuia kuenea kwa magonjwa, mfano ujenzi na matumizi ya vyoo, matumizi ya vifaa vya kunawa mikono, mifumo ya uondoaji majitaka na maji ya mvua, uondoaji maji machafu kwenye vituo vya kuchotea maji.

Afya (*Hygiene*) ni kitendo cha mtu kuweka mazingira yanayomzunguka yeye binafsi katika hali ya usafi, ili kuzuia kuenea kwa magonjwa, mfano matumizi ya maji yaliyo safi na salama, utunzaji wa maji, matumizi sahihi ya vyoo (ikiwemo kunawa mikono kwa kutumia maji safi na sabuni).



Usafi wa Mazingira: Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji ni Hatari kwa Afya.

4. Faida Za Afya na Usafi Wa Mazingira

Afya na Usafi wa Mazingira vinawezesha watumiaji wa maji kuwa na afya bora pamoja na kuwa na mazingira safi kutokana na yafuatayo:

- Kuepuka milipuko na kuenea kwa magonjwa kama kuharisha na kipindupindu
- Kuepuka uchafuzi wa maji

- Kulinda na kutunza miundombinu

Kuepuka milipuko na kuenea kwa magonjwa kama kuharisha na kipindupindu:

- Kutumia vyombo safi vya kuhifadhia maji

Kuepuka uchafuzi wa maji:

- Kutokuishi karibu na vyanzo, kutokufanya shughuli za kilimo, na ufugaji karibu na chanzo.

Kulinda na kutunza miundombinu:

- Miundombinu ya kulindwa na kutunzwa ni pamoja na Vyanzo vya maji, matanki ya kuhifadhi maji, mabomba ya kusambazia maji na vituo vya kuchotea maji.

5. Njia Bora za Afya na Usafi Wa Mazingira

Usafi wa Mazingira:

- Ukaguzi wa mara kwa mara na ukarabati wa miundombinu
- Kuweka uzio kuzunguka miundombinu, na kuifanyia usafi
- Kujengea sakafu ngumu na kuondoa maji machafu kwenye vituo vya kuchotea maji

Afya (Hygiene):

- Kutumia maji yaliyo safi na salama
- Kutumia vyombo safi na vyenye mfuniko kuhifadhia maji


Majumbani

- Kutumia vyoo bora
- Kunawa mikono kwa sabuni kabla na baada ya matukio muhimu

Aina za vyoo:

- Vyoo visivyo bora
- Vyoo bora

Afya yako iko mikononi mwako



Osha mikono yako kwa maji na sabuni

kila unapotumia choo

baada ya kumtawaza
mtoto

kabla ya kuandaa
chakula na kabla ya kula

unapo maliza kumhudumia
mgonjwa